RISALA YA MWENYEKITI WA BODI YA WADHAMINI YA HIFADHI ZA BAHARI NA MAENEO TENGEFU, PROF. YUNUS .D. MGAYA KATIKA KILELE CHA MAADHIMISHO YA MIAKA 10 YA HIFADHI ZA BAHARI NA MAENEO TENGEGFU TAREHE 23 AGOSTI 2005 UTENDE MAFIA.

Mheshimiwa Arcardo Ntagazwa Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais anayeshughulikia Mazingira
Mheshimiwa Ditopile Mzuzuri Mkuu wa Mkoa wa Pwani
Mwakilishi wa Katibu Mkuu – Wizara ya Maliasili na Utalii
Wajumbe wa Bodi ya Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu
Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Ushauri ya Hifadhi za Bahari ya Mafia
Mheshimiwa Mkuu Wa Wilaya ya Mafia
Wakurugenzi na Wakuu wa Taasisi za Ndani na za Kimataifa
Waheshimiwa Viongozi wa Dini na Siasa
Meneja na Watumishi wote wa Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu
Ndugu wananchi,
Itifaki imezingatiwa
Mabibi na Mabwana.

Ndungu Mgeni rasmi.

Kwanza kabisa kwa niaba ya Bodi na Uongozi mzima wa Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu tunapenda kuwakaribisheni katika hafla hii ya kuadhimisha miaka kumi ya Kuanzishwa rasmi Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu. Kuwepo kwenu hapa kunaonesha jinsi mnavyoguswa na suala zima la uhifadhi wa mazingira ya Bahari na raslimali zilizomo. Karibuni sana!

Miaka kumi imepita tangu Hifadhi Za Bahari zianzishwe rasmi mnamo Julai 1995. Hifadhi yetu ya Kwanza ilikuwa Hifadhi ya Bahari ya Kisiwa cha Mafia – HIBAMA ambapo kilele cha maadhimisho haya yanafanyika.

Ndugu Mgeni rasmi, Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu ni maeneo maalum kwenye mwambao wa bahari yetu au maji makuu ambayo kutokana na umuhimu wake kiokologia, bioanuai pamoja na utajiri wa raslimali za asili zilizomo ndani yake hutengwa kwa lengo la kulinda, kuhifadhi, kuendeleza na kusimamia rasilimali hizo kwa nia ya kudumisha utajiri huo kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vijavyo.

Tofauti baina ya mifumo hii miwili ni katika usimamizi. Kwenye maeneo tengefu matumizi pekee ambayo huruhusiwa ni yale yasiyoambatana na uvunaji wakati kwenye hifadhi za bahari matumizi mbali mbali ya uvunaji ikiwa ni pamoja na makazi ndani ya eneo la hifadhi huruhusiwa kupitia mpango maalum wa usimamizi inayotayarishwa kwa kuwashirikisha wadau wote ndani ya eneo husika.

Hatua hii ya kuanzisha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu ilifikiwa baada ya kubainika kuwa mazingira ya bahari yetu yalikuwa hatarini kuharibika kabisa kutokana na mbinu za uvuvi usio endelevu na uharibifu wa mazingira. Na hivyo Serikali ilichukua hatua za kuweka chombo ambacho kitahusika moja kwa moja kuweka usimamazi madhubuti wa maeneo hayo. Hadi sasa tunazo Hifadhi saba yaani Hifadhi ya Bahari ya Mafia yenye ukubwa wa eneo la mraba 822 kilometa, Hifadhi ya ya Ghuba ya Mnazi na Maingilio ya Mto Ruvuma yenye eneo la mraba 650, Maeneo tengefu manne ya Dar es Salaam na Maziwe. Pia vipo visiwa vidogo vidogo ambavyo havikaliwi na watu ambavyo vipo mbioni kupewa nguvu ya sheria kuwa Maeneo Tengefu. Aidha jumla ya wakazi wapatao 47,000 katika vijiji 28 wanaishi ndani ya maneo ya Hifadhi za Bahari.

1. MADHUMUNI MAKUBWA YA KUANZISHA HIFADHI ZA BAHARI NA MAENEO TENGEFU NI:-

i) Kulinda na kuhifadhi michakato kwenye maeneo yenye mkusanyiko mkubwa wa bioanuai pamoja mifimo ya ikolojia ya baharini na mwambao wa pwani.

ii) Kuhamasisha wananchi kutumia kwa busara rasilimali ambazo hazitumiki kabisa au hazitumiki kikamilifu kwa sasa.

iii) Kusimamia maeneo ya bahari na mwambao wa pwani ili kuwezesha matumizi endelevu ya rasilimali na ukarabati wa maeneo yaliyo haribiwa.

iv) Kuhakikisha kuwa wananchi walio wakazi ndani ya hifadhi wanashirikishwa katika nyaja zote za upangaji, uendelezaji na usimamizi wa hifadhi na maeneo tengefu, wananufaika wanashirikishwa katika manufaa yatokanayo na hifadhi na wanapewa kipaumbele katika matumizi ya rasilimali na fursa za kiuchumia zinazojitokeza.

v) Ukuzaji wa elimu ya mazingira na usambazaji wa taarifa kuhusu uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali kwenye hifadhi za bahari na maeneo tengefu

vi) Kuwezesha kufanyika kwa tafiti, ufuatiliaji na kutathimini hali ya matumizi ya rasilimali

Tangu tupewe majukumu hayo mwaka 1995 tumeweza kuyatekeleza kwa umakini mkubwa kama ifuatavyo:

2. UHAMASHISHAJI ,ELIMU KWA JAMII NA UPASHANAJI HABARI:

Mkakati wa kwanza ulikuwa uhamasishaji na upashanaji wa habari. Kazi hii ilionekana ifanyike kwanza ili tujiweke katika nafasi ya kuelewana na kufahamiana nini tunatakiwa tufanye, kwa nini na pia wajibu wa kila mmoja wetu katika kuhifadhi maeneo tete ambayo ni chimbuko la uzalishaji wa samaki na viumbe wengine wa bahari, itakumbukwa kuwa uharamia wa kutumia baruti ulikuwa umeshamili sana. Ilibidi tuimarishe njia za mawasiliano na kutumia mbinu mbalimbali za kufikishiana ujumbe, kwa hiyo:

- Utaratibu wa upashanaji habari kwa kupitia vikao vya mara kwa mara na radio za upepo (Ra dio calls) umewekwa. Tuliweka redio kwenye kila kijiji au maeneo maalum. Kwa kutumia redio hizo wananchi wamekuwa kupasishana habari si kwa ajili ya ulinzi na usimamizi wa rasilimali zilizomo ndani ya hifadhi pekee bali pia mawasiliano ya kawaida kati ya sehemu moja hadi nyingine. Kwa kutambua na kusaidia uhifadhi endelevu Kampuni ya simu za mkononi ya Vodafone (UK) kupitia WWF imewezesha kupatikana kwa huduma za simu za mkononi kupitia kampuni ya Vodacom (TZ) wilayani Mafia. Kampuni ya Celtel nayo imetuunga Mkono kuweka Mtandao wa simu za Mkononi Wilayani Mafia. Mitandao hii iliwekwa si kwa masilahi ya kiuchumi bali kuwezesha shughuli za jamii na huifadhi wa mazingira.

- Jamii na wadau mbalimbali wamekuwa wakielimishwa na kujulishwa mambo mbalimbali yahusuyo hifadhi kupitia machapisho mbalimbali kama vile vijalida, *posters*, vipeperushi, fulana, picha za kuchora na kupigwa. Aidha tulianzisha jarida la Dodoji ambalo uchapishwa mara kwa mara kama njia ya kuelimisha jamii juu ya shughuli za uhifadhi. Makala mbali mbali kuhusu hifadhi zetu zimekuwa zikichapishwa kwenye magazeti na TV na kusambazwa kwa wadau.
- Wadau kupitia mikutano, semina, warsha na majadiliano ya kila wakati na watumishi wa Hifadhi wameweza kupashwa habari zinazohusu hifadhi na wao kutoa mawazo na michango yao.
- Kumekuwepo na maonyesho ya filamu mbalimbali za video zinazohusu utunzaji wa mazingira ya bahari ambazo zimekuwa zikionyeshwa kwa wadau mbalimbali.

- Tumejenga vituo vya upashanaji Habari kwenye Maeneo Tengefu ya Dar es salaam

.

- Mkakati na mpango wa Elimu ya Mazingira umeandaliwa na kwa kushirikiana na Mradi wa Usimamizi wa Pwani (TCMP) ulioko chini ya Baraza la Taifa la Kusimamia Mazingira (NEMC) kupitia mpango wa Green Com na pia mpango wa elimu ya Mazingira kushirikiana na WWF tumekuwa tukitoa tuzo za utunzaji bora wa Mazingira kupitia mashindano ya kila mwaka kwa wanaofanya vizuri katika suala la uhifadhi.kwenye siku ya maadhimisho ya mazingira ya dunia. Tuzo hizo kama vile baiskeli nk zimekuwa chachu ya kuamsha ari ya kulinda mazingira ya Bahari.Mkakati huu umezingatia nafasi ya makundi yote yakiwemo mashule, vikundi vya wanawake, wazee, wasimamizi wa sheria na watumiaji wa rasilimali.

- Kitabu cha muhtasari na kiongozi cha mwalimu juu ya elimu ya mazingira vimeandaliwa Tunasubiri kibali toka kwa uongozi wa elimu mkoa Mtwara ili kuanza kutumika kwa darasa la tano mpaka la saba kwa shule zilizomo ndani ya hifadhi kwa majaribio.

3. USHIRIKISHWAJI WA JAMII KATIKA MPANGO WA USIMAMIZI WA RASILIMALI

Katika kutekeleza wajibu huu tuliweza kusimika asasi zote zilizoanshishwa kwa mujibu wa sheria na 29 ya 1994 Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu. Kwa hiyo

- Kamati za Hifadhi na Ulinzi za vijiji zimeundwa katika vijiji vyote vilivyomo ndani ya hifadhi. Kamati hizi zinahusika kuratibu shughuli za wakazi ndani ya Hifadhi.
- Kamati za ushauri za hifadhi zikiwa na wajumbe kutoka makundi mbali mbali ya jamii na wawakilishi wa wananchi na wafanyabiashara zimeanzishwa. Uteuzi wa wajumbe wa kamati hizi ulifanyika kidemokrasia na unazingatia rika na jinsia. Kamati hizi zimekuwa ni kiunganishi muhimu kati ya wananchi waishio ndani ya hifadhi, uongozi wa wilaya, uongozi wa hifadhi na bodi ya wadhamini. Aidha mipango yote ya hifadhi na maamuzi hufanywa na kamati hizi.
- Vikundi vya kulinda mazingira vya kujitolea vimeanzishwa katika kila hifadhi. Vikundi hivi pamoja na shughuli za kuweka mazingira katika hali ya ubora usimamia na kuthibiti uchafuzi wa mazingira, ukiukwaji wa kanuni na taratibu na pia kutoa ulinzi wa raslimali, wageni na mali zao.

4. KULINDA NA KUHIFADHI BIOANUAI NA MIFUMO YA IKOLOJIA

Katika kutekeleza jukumu hili, taasisi imekuwa ikishirikiana na wananchi na wadau mbali mbali kuweka mipango na miongozo mbali mbali ili kufanikisha ulinzi na uhifadhi na bioanuai zilizomo ndani ya Hifadhi na Maeneo Tengefu kama ifuatavyo:

- Jamii imehusishwa moja kwa moja katika shughuli za ulinzi na utunzaji wa rasilimali zilizopo katika maeneo yao.
- Tasisi pia imefanikiwa kuweka na kutekeleza miongozo ya tathmini ya athari kwa mazingira (EIA), mipango wa usimamizi wa utalii na mpango wa matumizi ya ardhi unaozingatia uhifadhi wa mazingira imetengenezwa.
- Kwa kupitia kamati za Hifadhi na kwa kushirikiana na Idara ya Uvuvi na jeshi Polisi. Hifadhi imeweza kuzuia uvuvi wa baruti kutokea milipiko zaidi ya 200 kwa wiki (1995) hadi sasa kuwa ni jambo la kihistoria.
- Jamii inahusishwa moja kwa moja katika shughuli za ulinzi na utunzaji wa rasilimali zilizopo katika maeneo yao. Uwezo wa jamii kushirikiana na hifadhi katika kufichua vitendo vya uhalifu umeongezeka. Karibu asilimia 50 ya wahalifu waliokamatwa tetesi za uhalifu huo ziliifikia Hifadhi toka kwa wanavijiji na pia wao kuhusika kuwatia nguvuni wahalifu hao.
- Baadhi ya vijana wamepewa mafunzo maalum ya ulinzi na utunzaji wa rasilimali na wanafanya kazi kama watunza hifadhi wa kujitolea. Watunza hifadhi wa kujitolea na wajumbe wa kamati za hifadhi walipelekwa katika Chuo cha Maliasili kwa jamii kilichopo Likuyu Sekamaganga mkoani Ruvuma na vilevile mafunzo mbali mbali hutolewa kwa njia ya mikutano, makongamano na warsha. Watunza hifadhi hawa wanachangia kwa kiasi kikubwa katika kuhakikisha jamii yote inajihusisha na suala la ulinzi wa rasilimali na utuzaji wa mazingira ya bahari na pwani.
- Katika kuhifadhi kasa na mazalia yake, wajumbe kutoka katika vijiji ambavyo pwani yake imetambuliwa kuwa na maeneo ya mazalia ya kasa kama vile Msimbati na Litembe (Mtwara) na Mchangani (Mafia) wanashiriki katika uhifadhi wa kasa.

5. KUENDELEZA MATUMIZI SAHIHI NA ENDELEVU YA RASILIMALI

Ili kukuza matumizi endelevu ya rasilimali shughuli mbali mbali ambazo si endelevu zimebainishwa na hivyo haziruhusiwi kufanyika ndani ya Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu. Ili kukabili hili tumefanya yafuatayo:

- Kwa kushirikiana na wadau,Hifadhi ilifanikiwa kutayarisha Mipango ya jumla ya usimamizi ya Hifadhi za Mafia, Ghuba ya Mnazi na Maeneo Tengefu ya DMRs. Utekelezaji wa mipango hii umewezesha kufanikisha juhudi za ulinzi na uhifadhi wa bioanuai na mifumo ya ikolojia.
- Kila kijiji ndani ya Hifadhi ya Ghuba ya Mnazi kimewezeshwa kuunda mpango wa usimamizi wa mazingira (VEMP), mchakato ulioshirikisha wanavijiji wote katika kila hatua. Mipango hii iliundwa kwa kushirikiana na wataalamu toka Halmashauri ya Wilaya ili kukipa kila kijiji uwezo wa kusimamia vyema rasilimali na mazingira ya kijiji chao.Hali kadhalika vijiji vimewezeshwa kuelewa hali halisi, ni wapi rasilimali gani ipo, na nini kinatakiwa kufanyika kwa rasilimali hizo ili zisimamiwe kiundelevu.
- Jamii imeshiriki katika kila hatua ya uandaaji wa mpango wa jumla wa usimamizi (GMP) ambapo katika mchakato huo suala la jinsia lilipewa kipaumbele na wanawake walishiriki toka kila kijiji.
- Wakazi ndani ya eneo la Hifadhi wanapewa kipaumbele katika matumizi ya rasilimali, ikiwa ni pamoja na kutengewa kanda, kama inavyoainishwa katika mpango wa jumla wa usimamizi (GMP).
- kutokana na kasi kubwa ya wawekezaji ambao wamevutiwa na eneo la hifadhi, Tumeandaa Tourism Investment Framework (TIF), IDP, Land Use Plan na Investment Guidelines ikiwa ni mkakati wa kukabiliana na shughuli za kimaendeleo ndani ya hifadhi.

- Hifadhi ya kisiwa cha Mafia ikishirikiana na WWF imetoa mikopo ya jumla ya Tshs 100,000,000 kwa vikundi 43 vyenye jumla ya wavuvi 169. Pamoja na mpango huu hifadhi pia imeanzisha mpango wa ubadilishanaji wa zana za uvuvi, majaribio ya jarife, wando dema, uvuvi wa mshipi wa kutumia karabai (light attraction) na kuweka vivutia samaki (FAD) umeanzishwa.

- Utaratibu wa kuviwezesha Vikundi vya Uvuvi umeandaliwa. Vikundi 2 vimewezeshwa kupata nyavu za dagaa na kuweza kuvua nje ya maeneo yaliyotengwa. Aidha Wavuvi wa jarife wamewezeshwa kuvua nje (bahari kuu) badala ya kuvua kwenye miamba ya matumbawe.

- Hatua za usimamizi zinazofaa katika kutunza na kuhifadhi maeneo ya kihistoria kama vile magofu ya Kua, Rasi Kisimani, Chole na ya kufanyia ibada zimeandaliwa kwa kushirikiana na Taasisi kama vile UNESCO, Chuo Kikuu na Idara ya Mambo ya Kale.

- Mafunzo kwa wanavijiji walioko katika maeneo ya kihistoria na ya kiutamaduni juu ya umuhimu na mahitaji ya usimamizi wa maeneo ya makumbusho.yametolewa zaidi ya wanaviji 134 wamenufaika na mafunzo hayo. Aidha vikundi 4 vyenye jumla ya vijana 60 wa mepewa mafunzo ya kuongoza watalii ili nao wafaidike na shughuli za utalii zinavofanyika katika hifadhi za bahari na maeneo tengefu.

- Kwa kushirikiana na WWF pamoja na wadau wengine wananchi wamehamasishwa kuanzisha vikundi vya maendeleo vya kuweka na kukopa (SACCOS). Hadi sasa kuna wanachama 748 wa vyama vya ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS) katika vijiji vyote 11 vilivyoko ndani ya hifadhi ya Kisiwa cha Mafia na wana mtaji wa jumla ya Sh.60,000,000/= unaozunguka.

6. KUENDELEZA RASILIMALI AMBAZO HAZITUMIWI

Tumebaini raslimali ambazo zimo ndani ya Hifadhi za Bahari ambazo hazijatumiwa lakini iwapo zitaendelezwa zinaweza kuwa chachu ya maendeleo kwa wakazi wa ndani ya Bahari na pia kupanua wigo wa shughuli mbadala badala ya kutegemea uvuvi pekee. Shughuli mbadala za kuingiza kipato ambazo ni endelevu zikiwemo ukulima wa mwani, ufugaji wa nyuki, kilimo cha mbogamboga, ufugaji wa samaki katika mabwawa na ufugaji wa chaza, kazi za mikono (usisi wa mikeka),na ufugaji wa mifugo kama mbuzi n.k. zilifanyiwa majaribio na zinatekelezwa kwa kushirikiana na wadau mbali mbali. Mbali ya kuendeleza matumizi endelevu shughuli hizi pia zitapelekea kupunguza shinikizo la matumizi ya rasilimali za baharini.Katika kufanya hivyo tumefanya yafuatayo:

- Ndani ya eneo la Hifadhi kuna mahoteli ya kitalii ambazo zimeibua fursa ya kutumia vivutio vya utalii na kuendeleza utalii wa bahari na burudani. Kwa sasa zipo hoteli sita katika Hifadhi za Bahari ya Mafia na Ghuba ya Mnazi. Aidha yapo mahoteli mengine kwenye mwambao wa Maeneo Tengefu ya Dar Es Salaam na Maziwe. Yapo mapendekezo ya kendeleza shughuli za utalii katika visiwa vidogo vidogo. Mwongozo wa kuwekeza katika maeneo hayo tete umekamilika. Yapo pia mapendekezo ya kujenga miradi endelevu ya utalii inayolenga soko la watu maarufu. Mradi wa uchimbaji wa gesi unaofanywa na kampuni ya Artumas Group and Partners kwenye Hifadhi ya bahari ya Ghuba ya Mnazi ni kivutio kikubwa cha uwekezaji ndani ya Hifadhi.Taarifa za awali zinaonyesha kuwa Ghuba ya Mnazi ina kiasi kikubwa cha gesi na hivyo kampuni hiyo ina mpango wa kuchimba visima vingine zaidi ndani ya Hifadhi.

    - Katika Kilimo na Mifugo majaribio ya kilimo cha michikichi na mipesheni yamefanyika, ufugaji wa kuku wa kienyeji na majogoo bora ulifanyika, maduka mawili ya pembejeo za kilimo yalifunguliwa na chanjo ya kuku kuzuia ugonjwa wa mdondo ilitolewa katika Hifadhi ya Mafia. Aidha shughuli za ufugaji wa mbuzi wa maziwa na kuku zimeainishwa na kutekelezwa ndani ya Hifadhi ya Ghuba ya Mnazi.

    - Kwenye Hifadhi ya kisiwa cha Mafia ukulima wa mwani umeongezeka toka tani 60 zenye thamani ya Tshs 7,200,000/= mwaka 2000 hadi kufikia tani 360 zenye thamani ya Tshs 79,200,000/= mwaka 2004. Ukulima wa mwani umekuwa ni ukombozi mkubwa kwa wananchi waishio ndani ya hifadhi katika kuinua hali zao za maisha hasa kina mama. Kutokana na mafanikio yaliyopatikana idadi ya wakulima pia imeongezeka kutoka wakulima 60 mwaka 2000 hadi kufikia zaidi ya wakulima 2004 mwaka huu.

    - Matokeo ya utafiti katika majaribio ya ufugaji wa nyuki yameonyesha kuwa asali inayozalishwa katika kisiwa cha Mafia ina ubora wa hali ya juu. Kutokana na utafiti huo wananchi na wadau wamehamasishwa ufugaji wa nyuki kwa lengo la kuongeza kipato cha mwananchi na kuchangia katika juhudi za kuondoa umaskini. Uhamasishaji huo umewezesha kumekuwepo na ongezeko la uzalishaji wa asali kutoka lita 20 zenye thamani ya Tshs.14,000/= kutoka mizinga 5 mwaka 1997 hadi kufikia lita 400 zenye thamani ya Sh. 1,200,000/= kutoka mizinga 109 mwaka 2005 kwenye Hifadhi ya Mafia. Shughuli hii inahamasihwa kwenye Hifadhi ya Mnazi Bay pia.

    - Kuendeleza jitahada za kina mama katika kukuza utamaduni na sanaa ya Mtanzania na kuongeza kipato cha familia kwa kusaidia vikundi vya kina mama wasusi wa mazulia na mikeka. Vikundi 4 vyenye jumla ya wanachama 43 vimeweza kuongeza uzalishaji toka mazulia 90 mwaka 2002 yenye thamani 207,500/= hadi kufikia mazulia 304 yenye thamani ya Tshs.942,000/= mwaka 2005.

    - Majaribio ya Kuzalisha Lulu yameonesha mafaniko makubwa. Majaribio ya awali yamezalisha lulu 143 zinazokadiriwa kuwa na thamani ya shs Milioni 7.
    - Wana kikundi katika Kijiji cha Mngoji wilayani mtwara wamewezeshwa kuchimba bwawa la kufugia samaki.

7. UFUATILIAJI NA UTAFITI

- Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu imekuwa ikishirikiana na taasisi mbali mbali za ndani na nje ya nchi kufanya tafiti na ufuatiliaji wa hali ya rasilimali, hali ya kijamii na kiuchumi ili kuziba pengo la mahitaji ya takwimu ambazo haziwezi kupatikana kwa ufuatiliaji wa ndani. Tafiti hizi ufanyika kwa kuwashirikisha wanajamii. Taasisi ambazo tumeshirikiana nao ni pamoja na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Taasisi ya Sayansi za Bahari (IMS) na Taasisi ya Utafiti ya Uvuvi nchini (TAFIRI), CORDIO, FRONTIER, Mpango wa Afrika wa utafiti wa Silikanti (ACEP), URI na kadhalika. Matokeo ya tafiti hizo yanasaidia Hifadhi kuweka mipango muafaka ya utekelezaji wa shughuli zake za kila siku kwa mfano uanzishwaji wa shughuli mbadala, utoaji wa elimu ya mazingira kwa jamii na uhimizaji wa matumizi endelevu ya rasilimali. Katika tafiti zote watafiti wamewezeshwa kwa kupatiwa vifaa vya ofisi na baharini,

watumishi wa kuongozana nao wakati wa utafiti wao na hata kuwaondolea ada za kiingilio katika Hifadhi ili kuwavutia kuja kufanya tafiti.

- Maeneo kipaumbele (priority areas) katika utafiti yamebainishwa na kusambazwa kwa watafiti
- Tafiti mbalimbali zilizofanyika zikiwa na lengo la kujua hali halisi ya rasilimali na uchumi jamii katika eneo la hifadhi ni pamoja na:

  Hali ya Matumbawe yaliyopo na hali yake, Aina za samaki wanaopatikana na maeneo yao, Utunzaji na uendelezaji wa upatikanaji wa kasa na nguva, Shughuli za uchumi jamii na njia mbadala za kujiongezea kipato, Mfumo wa shughuli za kijamii, Uvunaji wa matumbawe kwenye maeneo ya pembezoni mwa hifadhi, Mifano ashiria katika njia endelevu zilizo mbadala kwa ajili ya kujiongezea kipato, Anuai za mimea ya nchi kavu

Kulingana na matokeo ya awali, tafiti zinadhihirisha kuwa maeneo ya bahari katika eneo la Hifadhi yana viumbe wengi sana, na mandhari yake ni ya pekee nchini Tanzania na katika kanda yote kwa ujumla. Matokeo ya tafiti hizo ni pamoja na kuwapo kwa misitu ya mikoko yenye siha nzuri na afya njema ambayo inawezesha kuwepo maeneo mazuri ya mazalio ya samaki na viumbe wengine wa baharini kama kaa, kamba, uduvi,n.k.; maeneo makubwa ya nyasi bahari za aina mbalimbali yanayobadilika badilika na yenye uoto mzuri yapo kila mahali,aina za matumbawe magumu zisizopungua 250, aina 400 za samaki na karibu aina 100 za wanyama waishio majini.

8. UENDESHAJI WA HIIFADHI

- Katika uendeshaji wa Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu. Idadi ya watumishi imeongezeka kutoka mtumishi 1 mwaka 1995 hadi kufikia 48 mwaka 2005

- Vitendea kazi hususan vyombo vya baharini yaani maboti yameongezeka kutoka 1 mwaka 1995 hadi kufikia boti 12 mwaka 2005. Boti hizi zinatuwezesha kuwa baharini muda wowote ule tunapohitajika kufanya hivyo. Tumeongeza uwezo wetu wa kudhibiti na kusimamia shughuli za bahari kwa ufanisi mkubwa. Yapo maboti ya mwendo wa kasi kwa shughuli za doria na uokoaji. Kuwepo kwa vifaa hivi kumeifanya hifadhi kuwa chombo cha kutegemewa na wakazi pamoja na taasisi nyingine za serikali na za binafsi.

- Katika kipindi hiki tasisi imefanikiwa kupata majengo yetu wenyewe kwa ajili ya ofisi na nyumba kwa ajili ya watumishi. Tumejenga jengo kwa ajili ya shughuli za wananchi (Community Centre). Aidha vitendea kazi vimeongezeka na uwezo wa watumishi kufika maeneo ya vijiji na baharini umerahishwa kwa kiwango kikubwa kwa kupatikana magari, Boti na pikipiki.

Changamoto

Baadhi ya changamoto zinazozikabili Hifadhi za Bahari ni pamoja na

1. Uvuvi wa kutumia zana haribifu ndani na nje ya maeneo ya Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu.

2. Utegemezi mkubwa wa rasilimali za bahari na mwambao kwa wananchi waishio ndani na karibu Hifadhi.

3. Hali duni ya maisha kwa wananchi wengi waishio ndani ya Hifadhi na pembezoni mwa hifadhi pamoja na idadi kubwa ya watu wanaoishi ndani ya eneo la Hifadhi ambao wengi wao wanategemea raslimali za bahari kwa maisha yao ya kila siku ni tishio kwa raslimali zilizopo

4. Uelewa wa wadau mbalimbali kwenye masuala ya uhifadhi bado ni mdogo na kwa kutumia mapungufu haya baadhi ya makundi machache kuwaghiribu wananchi wasikubali kushiriki shughuli za Hifadhi. Mifano tunaiona katika vijiji vya Nalingu na Jibondo.

5. Makusanyo ya hifadhi bado ni ya chini jambo linalo pelekea misaada kwa jamii kuwa ni michache.

9. MATARAJIO YA BAADAE YA TAASISI

Kwa kuwa Taasisi imepewa jukumu la kuhakikisha maeneo yote yenye rasilimali muhimu za bahari yanahifadhiwa kwa manufaa ya vizazi vilivyopo na vijavyo majukumu makuu ya Taasisi katika kipindi kijacho yatakuwa kama ifuatavyo;

- Kuendelea na utambuzi na hatimaye kuyatangaza maeneo yenye sifa za kuingia katika mtandao wa Hifadhi za Bahari pamoja na visiwa vidogovidogo ambavyo havikaliwi na watu kwa kutumia taratibu zilizowekwa ili kuhakikisha kuwa matumizi endelevu ya rasilimali za bahari yanakuwepo na vivutio vya utalii vinasimamiwa vema

- Kuendelea na jitihada za kupanua wigo wa ajira na kipato cha wakazi waliomo ndani na wanaozunguka Hifadhi kupitia rasilimali zilizopo hususan uvuvi, utalii nk.

- Kuhakikisha Hifadhi za Bahari zinakuwa chanzo muhimu cha lishe bora kwa taifa kutokana na mazao yanayotokana na bahari.

- Kuimarisha upatikanaji na utoaji taarifa sahihi zinazohusu rasilimali na mwenendo mzima wa matumizi ya rasilimali katika maeneo ya hifadhi ili taarifa hizo ziwezeshe usimamizi na utoaji maamuzi kwa misingi ya kisayansi.

- Kuendeleza ushirikiana na mashirika ya kimataifa katika kufanya utafiti wa raslimali za bahari kama (ACEP)

Naomba kuwasilisha na ahsanteni sana kwa kunisikiliza.